



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**MWALIKO KWA WATAZAMAJI WA NDANI WA UCHAGUZI MDOGO
KATIKA JIMBO LA KONDE MKOA WA KASKAZINI PEMBA –ZANZIBAR
NA JIMBO LA USHETU**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika jimbo la Konde, Mkoa wa kaskazini Pemba na Jimbo la Ushetu tarehe 09 Oktoba, 2021

Kwa kuzingatia kanuni ya 18(3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kualika na kusajili Watazamaji wa uchaguzi wanaotaka kutazama uchaguzi.

Kupitia tangazo hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kualika taasisi na asasi mbalimbali nchini ambazo zinahitaji kutazama uchaguzi mdogo katika Majimbo ya Konde na Ushetu.

Asasi na taasisi zenyenye nia ya kutazama Uchaguzi huo zinatakiwa kuwasilisha maombi kwa kutumia Mfumo wa Menejimenti ya Watazamaji (OMS) kupitia “*link*” ifuatayo: <https://oms.nec.go.tz>

Barua ya maombi pamoja na mambo mengine itatakiwa kuainisha yafuatayo:-

- (i) Anuani kamili ya taasisi au asasi husika;
- (ii) Mahali au sehemu ambapo taasisi au asasi husika inafanyia kazi (Physical address);
- (iii) Shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;

- (iv) Sehemu ambazo asasi au taasisi inataka kufanya zoezi hilo la utazamaji.
- (v) Idadi ya watu ambao taasisi/asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao.
- (vi) Majina na namba za simu za viongozi wa taasisi au asasi husika kama yalivyoandikwa katika hati za usajili wa taasisi au taasisi.
- (vii) Ikiwataasisi au asasi inahusisha watendaji wa kimataifa wawili lazima wawe watanzania.
- (viii) Kuambatanisha nakala au kivuli cha hati ya usajili wa taasisi au asasi husika.
- (ix) Kuambatanisha nakala au kivuli cha Katiba ya taasisi au asasi husika.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 04 Septemba, 2021

Imetolewa leo tarehe 30/08/2021 na;



Dkt Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

Tarehe 30/08/2021.